# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS
## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MKOA WA DAR ES SALAAM

# MTIHANI WA UTAMILIFU KIDATO CHA SITA

# KISWAHILI - 1

**Msimbo: 121/1**

**Muda: saa 3:00** **Jumatano 5 Februari, 2025 Asubuhi**

mwalimu.com

**MAELEKEZO**

1. Karatasi hii ina jumla ya sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **nane (8)**.
2. Jibu maswali yote kutoka sehemu A na maswali matatu kutoka sehemu B, swali la tano (5) ni la lazima.
3. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
4. Andika **namba yako ya usajili** katika kila ukurasa wa karatasi zako za kujibia.

*Karatasi hii ina kurasa 3 zenye maandishi*

CamScanner

## SEHEMU A (Alama 40)

UFAHAMU NA UFUPISHO

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Soma kwa makini kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yanayofuata:-

Hapo zamani palikuwepo shujaa mmoja aliyeitwa Mkombozi. Siku nyingi zilikuwa zimepita tangu akikomboe kijiji chake kutokana na hujuma za majitu mawili. Aliliua jitu moja, lakini la pili lilinusurika na kukimbia.

Siku moja alifika kipusa aitwaye Chakisasi nyumbani kwake Mkombozi. Baada ya mazungumzo ya muda, Mkombozi aliona nyota yake ya jaha ilikuwa imeshuka. Alitaka kumuoa Chakisasi, naye akakubali. Wote wakaishi pamoja kama mme na mke.

Baada ya siku kadhaa, Chakisasi alimwomba mmewe amsindikize msituni kuchanja kuni. Mkombozi ambaye daima alichelea kumkatalia mkewe maombi yake alihiari. Wakafuatana unyounyo. Kila walipoufikia mti uliokauka, Chakisasi alisingizia, "Kuni zake si nzuri, hufuka moshi". Safari ya mwendo mrefu iliwafikisha kwenye msitu mkubwa tena wenye giza na milio ya kutisha. Hapo mkewe akasema, "Mkombozi, ikiwa wanipenda kweli, upande mti huu ili uniletee kilichomo katika kiota kile". Mkombozi aliparamia mti na alipofika juu aligeuka kwa pupa ili kumueleza mkewe kilichokuwamo katika kiota. Lo! Alishtuka kuona Chakisasi alikuwa amebadilika na kuwa jitu kubwa. Akakumbuka kisa cha miaka mingi iliyopita. Kiwewe kikamvaa. Akahisi siku zake zimefika ukingoni. Kwa sauti ya radi, jitu liliamuru, "Nitupie makinda hayo!" Mkombozi aliunyosha mkono uliokuwa ukitetemeka kuchukua wana wa ndege lakini mama yao alimsihi, "Nifae juani nikufae mvuani". Jitu lilichekelea kisha likanyanyua shoka kuanza kuukata mti. Lakini kila mti ulipoanza kuanguka kakakaka ndege aliuzunguka akinuizia maneno na mti ukajikita tena.

Haya yakaendelea mpaka ndege alipokaribia kuchoka. Ikasikika sauti kutoka shinani mwa mti ikisema, "Mkombozi tuokoe". Hapo ndipo ilimjia Mkombozi fikra, akaanza kuimba:

*Mbwa wangu Polisi, nateseka mno x 2*
*Mbwa wangu Baruti, nahangaika mno x 2*
*Mbwa wangu Fataki, nadhikika mno x 2*

Kwa mbali mbwa wa Mkombozi waliisikia sauti yake ya dhiki. Ikafuata vurumai ya mbwa kujitoa minyororoni. Hatimaye wakajinasua kufyatuka kama risasi. Wacha mbwa watifue vumbi!Kufumba na kufumbua, waliukaribia ule mti. Jitu lilipoona haya likajaribu kubadilika ili kuwa kisura tena, lakini bure!

Mbwa walilraruararua vipandevipande. Mkombozi alishuka akawasha moto mkubwa na kuteketeza vipande vya jitu. Hapo akarudi nyumbani na kuishi raha mstarehe na watu wake.

**Maswali**

a. Pendekeza kichwa cha habari kifaacho katika habari hii
b. Mkombozi alikuwa na faida gani kwa jamii yake? Taja faida mbili (2) tu.
c. Eleza sifa mbili (2) za Chakisasi
d. Nini maana ya msemo huu, "Nifae juani, nikufae mvuani" kama ulivyotumika katika habari hii.
e. Neno "jitu" limetumika katika hali gani?
f. Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika habari hii:-
   i. Lilinusurika
   ii. Nasua
   iii. Kipusa
   iv. Makinda
   v. Hujuma
   vi. Vurumai



CamScanner

2. Kwa kutoa mifano, eleza maana ya istilahi zifuatazo kama zinavyotumika katika lugha:-
   i. Mzizi
   ii. Kishazi tegemezi
   iii. Vimadende
   iv. Alomofu
   v. Shamirisho

3. Kwa kutumia mifano madhubuti, onyesha tofauti baina ya mofimu tegemezi na silabi katika lugha ya Kiswahili.

4. "Wataaluma mbalimbali hutumia mtindo wa lugha kwa namna ya pekee ili kufikisha ujumbe uliokusudiwa". Kwa kutumia hoja tano (5) fafanua usemi huu.

SEHEMU B

Jibu maswali **matatu (3)** katika sehemu hii. Swali la **tano (5)** ni la lazima.

5. (a) Wafasiri huweza kukumbana na vikwazo vinavyowakaba koo wanapoendelea na kazi ya kufasiri. Kwa kutumia hoja tano (5) eleza vikwazo vinavyoweza kupelekea tafsiri tenge.

   (b) Kwa kutumia tafsiri ya kimawasiliano, tafsiri sehemu ya wimbo wa taifa la Tanzania kutoka lugha chasili kwenda lugha lengwa ya Kiingereza.

**WIMBO WA TAIFA**

Mungu ibariki Tanzania
Wabariki viongozi wake
Hekima, umoja na amani
Mungu ibariki Tanzania
Na watu wake
Ibariki Tanzania
Ibariki Tanzania
Tubariki watoto wa Tanzania.

6. BAKITA kama mwili wa mwanadamu wenye mifumo mbalimbali ya utendaji kazi kwa kushirikiana pamoja. Kwa kutumia dai hili, fafanua idara tano (5) zinazounda baraza hilo.

7. Kwa kutumia mifano, eleza maana na muundo wa wasifukazi kisha andika wasifu wako kama mwombaji wa kazi ya kuhariri habari katika kampuni ya Mwananchi iliyopo jijini Dar es salaam, S.L.P 33360.

8. Nini maana ya usanifishaji? Eleza umuhimu wa usanifishaji (hoja tatu) kisha hatua zilizofuatwa katika usanifishaji wa lugha ya Kiswahili.



CamScanner